TANGAZO LA SERIKALI Na. 312 lililochapishwa tarehe 31/07/2015

SHERIA YA DAWA NA VIFAA TIBA,
(SURA 219)

**KANUNI**

*( Zimetengezwa chini ya kifungu cha 122 (1) (e))*

# KANUNI ZA USAJILI WA MAJENGO, UINGIZAJI NA USAFIRISHAJI NJE YA NCHI WA DAWA NA MALIGHAFI, 2015

MPANGILIO WA KANUNI


*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

1. Jina
2. Matumizi
3. Tafsiri

SEHEMU YA PILI
USAJILI WA MAJENGO

4. Usajili wa majengo
5. Utaratibu wa kusajili majengo
6. Masharti ya usajili wa majengo
7. Ukaguzi wa majengo
8. Utoaji wa cheti cha usajili na kibali cha biashara
9. Kubatilisha, kusimamisha na kufuta cheti cha usajili na kibali
10. Utunzaji kumbukumbu na nyaraka
11. Taarifa ya mabadiliko ya jina na msimamizi
12. Masharti ya uuzaji wa dawa kutoka nje ya nchi
13. Kusitisha biashara

SEHEMU YA TATU

UINGIZAJI NA USAFIRISHAJI NJE YA NCHI WA DAWA NA MALIGHAFI


14. Masharti kwa mwingizaji na msafirishaji nje ya nchi
15. Masharti ya kuingiza au kusafirisha nje ya nchi
16. Maombi ya vibali vya kuingiza au kusafirisha nje ya nchi
17. Utoaji wa vibali vya kuingiza au kusafirisha nje ya nchi
18. Vibali vya dawa za tiba zenye asili ya kulevya
19. Vituo vya forodha
20. Masharti ya uingizaji na usafirishaji nje wa dawa za matumizi binafsi
21. Masharti ya dawa za msaada
22. Uingizaji wa sampuli za dawa zisizouzwa
23. Uingizaji wa dawa zisizotozwa
24. Maombi ya kuingiza dawa za majaribio
25. Muda wa matumizi wa dawa zinazoingizwa nchini
26. Uwekaji wa lebo kwenye dawa na malighafi zinazoingizwa nchini
27. Kubatilisha, kufuta au kusimamisha kibali cha kuingiza au kusafirisha nje ya nchi
28. Ukaguzi wa shehena katika vituo vya forodha
29. Uchukuaji wa sampuli
30. Kukataa au kuzuia shehena


SEHEMU YA NNE
MASHARTI YA JUMLA


31. Pingamizi
32. Rufaa
33. Makosa na adhabu
34. Kufifilisha makosa


---

MAJEDWALI

---

SHERIA YA DAWA NA VIFAA TIBA,
(SURA 219)

**KANUNI**

*( Zimetengezwa chini ya kifungu cha 122 (1) (e))*

KANUNI ZA USAJILI WA MAJENGO, UINGIZAJI NA USAFIRISHAJI NJE YA NCHI WA DAWA NA MALIGHAFI, 2015

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

Jina

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Usajili wa Majengo, Uingizaji na Usafirishaji Nje ya Nchi wa Dawa na Malighafi za mwaka 2015.

Matumizi

**2**. Kanuni hizi zitatumika katika usajili wa majengo ya dawa za binadamu na mifugo, uingizaji na usafirishaji nje ya nchi wa dawa na malighafi ndani ya Tanzania Bara.

Tafsiri

**3**. Katika Kanuni hizi, isipokuwa muktadha ukihitaji vinginevyo -

Sura 219

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba au kwa kifupi TMDA iliyoundwa chini ya kifungu namba 4 (1) cha Sheria;

"kibali cha biashara" maana yake ni kibali kinachotolewa kwa mwaka au kibali kinachotolewa kwa mwingizaji au msafirishaji wa dawa nje ya nchi ili kumruhusu kufanya biashara ya uingizaji au usafirishaji";

"Mamlaka yenye dhamana" maana yake ni Wizara au Idara yenye dhamana ya afya

au Mamlaka ya udhibiti wa dawa ya nchi ambapo dawa inatoka;

"dawa za tiba zenye asili ya kulevya" maana yake ni dawa au kemikali bashirifu zenye viambata hai vya kulevya kama ilivyotafsiriwa kwenye Sheria;

"cheti cha dawa za msaada" maana yake ni cheti kinachotolewa kutoka mamlaka yenye dhamana ya nchi dawa inapotoka kuthibitisha msaada;

"kibali cha kusafirisha nje ya nchi" maana yake ni kibali kinachotolewa na Mamlaka kwa msafirishaji nje ya nchi kumruhusu kusafirisha dawa;

"msafirishaji nje ya nchi" maana yake mtu au taasisi iliyoidhinishwa chini ya Kanuni hizi kusafirisha dawa nje ya nchi;

"sampuli za dawa zisizouzwa" maana yake ni dawa zinazotumika kwa lengo la kuitangaza dawa;

"bidhaa au dawa zisizotozwa" maana yake ni bidhaa zilizopunguziwa bei;

"mwingizaji" maana yake ni mtu au taasisi iliyoidhinishwa chini ya Kanuni hizi kuingiza dawa kwa lengo la kuuza, kugawa kwa kuuza, kusambaza, kutoa msaada au kutumika Tanzania;;

"kibali cha uingizaji" maana yake ni kibali kinachotolewa na Mamlaka kwa mtu au taasisi kuingiza dawa au malighafi nchini Tanzania;

"mkaguzi" maana yake ni mkaguzi aliyeteuliwa, kuidhinishwa au kutambuliwa kwa mujibu wa Sheria;

"dawa za majaribio" maana yake ni dawa zenye viambata hai au bila viambata zinazofanyiwa majaribio na zinajumuisha dawa zilizosajiliwa ambazo zinatumika au kutengenezwa tofauti na zilivyosajiliwa au kwa matumizi tofauti ili kupata taarifa zaidi ya matumizi yake;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya afya kwa wakati huo;

"Mmiliki wa dawa" maana yake ni mtu au kampuni ambayo imesajili dawa kwa jina lake;

"dawa" maana yake ni dawa kama ilivyotafsiriwa kwenye Sheria;

"cheti cha dawa" maana yake ni maelekezo ya kitaalam ya daktari wa binadamu, mifugo au meno yanayotambulika kisheria kwa ajili ya kuelekeza utayarishaji na utoaji wa dawa kwa mtaalam wa dawa;

"kituo cha forodha" maana yake ni kituo kinachotambuliwa kuingizia na kusafirishia dawa na malighafi nje ya nchi kama ilivyo katika Kanuni ya 10 (2);

"majengo" maana yake ni ardhi, miundo ya ujenzi, vyumba vya chini na vyombo, na kuhusiana na jengo ni pamoja na sehemu yoyote ya jengo, yadi au mahali pa

kuhifadhia, na kuhusiana na chombo maana yake ni meli, mashua, ndege na inajumuisha chombo cha kubebea au kipokezi cha aina yoyote;

Sura 311
Sura 319

"msimamizi" maana yake ni mfamasia au daktari wa mifugo mwenye jukumu la kusimamia uingizaji au usafirishaji nje ya nchi kama alivyosajiliwa chini ya Sheria ya Famasi au Sheria ya Mifugo;

"malighafi" maana yake ni kitu chochote chenye ubora uliothibitishwa kutumika katika utengenezaji wa bidhaa za dawa, isipokuwa vifungashio; na

"kifungashio" maana yake ni kitu chochote ikiwa ni pamoja na kilichochapishwa kinachotumika kufungashia za dawa, isipokuwa kifungashio cha nje kinachotumika kwa ajili ya kusafirishia mizigo ya dawa. Kifungashio kinaweza kutambuliwa kama kifungashio cha awali au cha pili kutegemea kama kinagusana moja kwa moja na dawa au la.

## SEHEMU YA PILI
## USAJILI WA MAJENGO

Usajili wa majengo

**4.-** Mtu hatahifadhi kwa kuuza au kumiliki dawa isipokuwa katika majengo yaliyosajiliwa chini ya Sheria au sheria nyingine yoyote inayotumika kwa sasa.

Maombi ya usajili wa majengo

**5.-** (1) Maombi ya usajili wa majengo ya dawa zinazodhibitiwa chini ya Sheria yatawasilishwa kwa Mamlaka kwa kutumia Fomu iliyoainishwa katika **Jedwali la Kwanza** la Kanuni hizi na kulipiwa ada kama ilivyoainishwa katika Kanuni ya Ada na Tozo zinazotumika kwa wakati huo.

(2) Bila kuathiri masharti ya jumla ya kanuni ndogo ya kwanza (1), maombi yataambatana na:

(a) nakala ya mkataba uliosainiwa kati ya mwombaji na Msimamizi pale inapobidi; na
(b) nakala ya leseni ya mfamasia au daktari wa mifugo kama msimamizi.

Masharti ya usajili wa majengo

**6.-** (1) Jengo litasajiliwa ikiwa linakidhi masharti yafuatayo:

(a) liko mbali na maeneo au shughuli zinazochafua hewa, maji taka, au mahali pengine popote ambapo usalama, ubora na ufanisi wa bidhaa za dawa unaweza kuathirika;
(b) lina anuani ya posta au mahali ambapo biashara inafanywa, na taarifa hizi zijazwe kwa uwazi katika fomu ya maombi;

Sura 212

(c) mmiliki wa jengo ana namba ya utambulisho wa mlipa kodi na amesajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Usajili wa Biashara;
(d) litakuwa la kudumu, salama na kujengwa kwa vifaa vya kudumu, kuezekwa na mabati, kuwa na sakafu yenye saruji, marumaru au terazo na kuta zilizo rahisi kusafishika ili kulinda dawa zilizohifadhiwa ndani yake;
(e) litawekewa vifaa kinga dhidi ya panya, ndege na wadudu;
(f) liwe na vyumba vilivyopakwa rangi nyeupe au nyingine yoyote inayoweza kuonesha uchafu na rahisi kuosheka;
(g) mazingira yake yanatunzwa ili kupunguza vumbi na uchafu mwingine kuingia katika jengo;
(h) liwe na mwanga wa kutosha, mzunguko wa hewa na jotoridi lisilozidi nyuzi 30 kuwezesha shughuli kufanyika;
(i) limewekewa miundombinu ya kuzuia wizi na kuingia bila idhini;
(j) liwe na alama na maneno yaliyoandikwa "USIVUTE SIGARA AU TUMBAKU" yanayoonekana wazi kwenye mlango au eneo;
(k) lina vifaa sahihi vya uhifadhi na utunzaji ili kuhakikisha usalama wa dawa;
(l) lina kabati au eneo maalum la kuhifadhia dawa za tiba zenye asili ya kulevya;
(m) liwe na eneo lenye ukubwa usiopungua mita za mraba 40 na urefu usiopungua mita 2.5 na liwe na vyumba vya kupokea, kuhifadhi, kuweka kumbukumbu na mlango mmoja tu wa kuingilia; na
(n) jina la biashara linalopendekezwa lisipotoshe watumiaji wa dawa au kukiuka kifungu chochote cha Sheria au sheria nyingine yoyote ya nchi.

Ukaguzi wa majengo

**7.-** (1) Baada ya kupokea fomu ya maombi ya usajili wa jengo iliyokamilika, Mamlaka itafanya ukaguzi wa jengo ili kuhakikisha linatimiza masharti kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(2) Wakati wa kufanya ukaguzi wa jengo chini ya kanuni ndogo (1), Mamlaka itatumia dodoso la ukaguzi litakalotumika kama mwongozo wa usajili wa majengo.

Utoaji wa cheti cha usajili na kibali cha biashara

**8.-** (1) Mamlaka inaweza, ikiwa imeridhika kuwa masharti yaliyoainishwa katika Kanuni hizi yametimizwa, kusajili jengo na kutoa cheti cha usajili kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali la Pili**

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), mtu yeyote hataruhusiwa kuanza

biashara katika eneo lililosajiliwa hadi atakapokuwa amepata kibali cha biashara kutoka Mamlaka.

(3) Kibali cha biashara kilichotolewa chini ya kanuni ndogo ya (2) kitakuwa kama ilivyoainishwa katika **Jedwali la Tatu** na kitaisha muda wake wa matumizi tarehe 30 Juni ya kila mwaka.

(4) Mtu yeyote hataruhusiwa kuhamisha au kutumia cheti au kibali cha biashara kilichotolewa chini ya Kanuni hizi, kwa mtu mwingine yeyote au njia nyingine tofauti na kusudi lililotolewa isipokuwa kwa kutoa taarifa na kupata idhini ya Mamlaka.

Kubatilisha, kusimamisha na kufuta cheti cha usajili na kibali

**9.-** Mamlaka inaweza, kwa sababu za msingi kusimamisha, kubadilisha, kufuta au kubatilisha cheti cha usajili wa jengo na kibali cha biashara.

Utunzaji kumbukumbu na nyaraka

**10.-** (1) Kila mmiliki anapaswa kuwa na taarifa zifuatazo kwenye jengo lake:

(a) mfumo unaofaa kudhibiti taarifa za dawa;
(b) kumbukumbu za ukaguzi;
(c) kitabu cha kushughulikia malalamiko;
(d) rejesta ya dawa zilizochina;
(e) rejesta ya dawa za tiba zenye asili ya kulevya;
(f) rejesta ya taarifa za uondoaji wa dawa katika soko;
(g) rejesta ya wateja yenye taarifa za jina, anuani ya posta, barua pepe, namba ya simu, namba ya usajili wa jengo, jina la msimamizi wa jengo na namba yake ya usajili; na

TS. 363

(h) taarifa nyingine zozote kama ambavyo imeainishwa kwenye Kanuni za Utunzaji na Usambazaji Bora wa Dawa na Vifaa Tiba zinazotumika.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), mwingizaji wa dawa nchini au msafirishaji nje ya nchi anapaswa kutunza nyaraka zifuatazo:

(a) ankara kifani za mwisho na vibali vyake;
(b) nakala za ufikishaji mizigo;
(c) ankara za mauzo;

(3) Nyaraka zilizotajwa katika kanuni ndogo ya (2), zitapaswa kuhifadhiwa na kutunzwa ndani ya jengo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja (1) baada ya tarehe ya kuisha muda wa matumizi ya dawa.

Taarifa ya

**11.-** Taarifa ya mabadiliko yoyote ya jina, umiliki, msimamizi au

mabadiliko ya jina na msimamizi

mabadiliko mengine yanayohusu jengo lililosajiliwa itawasilishwa kwa Mamlaka.

Masharti ya uuzaji wa dawa kutoka nje ya nchi

**12.-** Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi, mwingizaji wa dawa nchini anapaswa kuuza dawa kwa jumla.

Kusitisha biashara

**13.-** (1) Endapo mmiliki anatarajia kusitisha biashara yake kwa sababu yoyote, atatakiwa kuitaarifu mapema Mamlaka, ili utoaji wa dawa ufanyike chini ya usimamizi wa Mamlaka.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), mmiliki atapaswa ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya kufutwa; kusalimisha kwa Mamlaka cheti cha usajili wa jengo lake au kibali kilichofutwa, kadri itakavyokuwa.

## SEHEMU YA TATU
## UINGIZAJI NA USAFIRISHAJI NJE YA NCHI WA DAWA NA MALIGHAFI

Masharti kwa mwingizaji na msafirishaji nje ya nchi

**14.-** (1) Mtu yoyote hataruhusiwa kuingiza au kusafirisha nje ya nchi dawa au malighafi hadi atakapotimiza masharti yafuatayo:

(a) ana mfamasia aliyesajiliwa na Baraza la Famasi ambaye atakuwa ndiye msimamizi wa biashara;
(b) ikiwa jengo ni la biashara jumla ya dawa za mifugo, awe na daktari wa mifugo aliyesajiliwa na Baraza la Veterinari;
(c) ana jengo lililosajiliwa na Mamlaka;
(d) ana kibali hai cha biashara;

(2) Bila kujali kanuni ndogo (1), uingizaji wa malighafi au vifungashio utaruhusiwa kwa wazalishaji wa dawa pekee.

Masharti ya kuingiza au kusafirisha dawa nje ya nchi

**15 .-** (1) Mtu yeyote hataruhusiwa kuingiza au kusafirisha nje ya nchi dawa au malighafi mpaka awe na kibali hai kilichotolewa na Mamlaka.

(2) Mtu yeyote hataruhusiwa kuingiza dawa ambazo hazijasajiliwa na Mamlaka.

(3) Bila kujali kanuni ndogo (1) na (2) Mamlaka inaweza kuidhinisha, kwa ombi la mtu yeyote au taasisi na kwa maslahi ya umma, uingizaji wa dawa ambazo hazijasajiliwa.

Maombi ya vibali vya kuingiza au kusafirisha nje

**16.-** (1) Maombi ya kibali cha kuingiza dawa nchini yatawasilishwa kwa njia ya kielektroniki kwa kutumia fomu iliyoainishwa katika **Jedwali la Nne** la Kanuni hizi.

ya nchi

(2) Maombi ya kibali cha kusafirisha dawa nje ya nchi yawasilishwe kwa njia ya kielektroniki kwa kujaza fomu iliyoainishwa kwenye **Jedwali la Tano** la Kanuni hizi.

(3) Maombi chini ya kanuni ndogo ya (1) na (2) ambayo yatawasilishwa kielektroniki yatapaswa kujazwa kiukamilifu na kuwekewa muhuri, tarehe na saini ya msimamizi wa biashara.

(4) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (3), ankara kifani itapaswa kuwa na taarifa zifuatazo:

(a) jina na anuani ya mshitiri;
(b) jina na anuani ya mtengenezaji wa dawa;
(c) jina la kibiashara la dawa;
(d) jina halisi la dawa na nguvu yake;
(e) kwa dawa ambazo zina kiambata hai zaidi ya kimoja, jina la kila kiambata hai na nguvu yake viainishwe;
(f) viwango vilivyotumika wakati wa utengenezaji wa dawa;
(g) nambari ya usajili wa dawa iliyotolewa na Mamlaka;
(h) kiasi, ukubwa wa pakiti, thamani ya kila pakiti na jumla ya thamani kwa fedha inayobadilishika;
(i) nambari ya toleo au loti;
(j) tarehe ya kutengenezwa na muda wa kuisha matumizi ya dawa;
(k) njia ya usafirishaji kama maji, anga au nchi kavu;
(l) kituo cha forodha kilichoidhinishwa; na
(m) saini na muhuri wa mshitiri.

Utoaji wa vibali vya kuingiza au kusafirisha nje ya nchi

**17.-** (1) Mamlaka inaweza kutoa kibali cha kuingiza au kusafirisha dawa nje ya nchi, endapo itaridhika kuwa masharti yaliyowekwa katika Kanuni hizi yametimizwa ikiwa ni pamoja na tozo husika kulipwa kama ilivyoainishwa kwenye kanuni za ada na tozo zinazotumika.

(2) Kibali cha kuingiza dawa nchini chini ya kanuni ndogo ya (1) kitakuwa kama ilivyoainishwa katika **Jedwali la Sita** la Kanuni hizi.

(3) Kibali cha kusafirisha dawa nje ya nchi chini ya kanuni ndogo ya (1) kitakuwa kama ilivyoainishwa katika **Jedwali la Saba** la Kanuni hizi.

(4) Muda wa uhai wa kibali cha kuingiza dawa nchini utakuwa miezi sita na kwa kibali cha kusafirisha dawa nje ya nchi miezi mitatu kutoka tarehe ya kutolewa kwake.

(5) Kibali cha kuingiza au kusafirisha dawa nje ya nchi kitatumika kwa shehena

moja tu na hakipaswi kuhamishwa kwa mtu mwingine.

(6) Ikiwa shehena moja itahitaji kusafirishwa zaidi ya mara moja, kibali kimoja kinaweza kutumika kwa shehena zisizozidi tatu;

Vibali vya dawa za tiba zenye asili ya kulevya

**18. -** (1) Kwa kuzingatia masharti mengine ya Kanuni hizi, kibali cha kuingiza au kusafirisha nje ya nchi dawa za tiba zenye asili ya kulevya kitatolewa pamoja na cheti cha kuingiza dawa hizo kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali la Nane** la Kanuni hizi na kibali cha dawa za Saiktropiki kitatolewa katika karatasi ya rangi ya pinki na kibali cha dawa za Nakotiki kitatolewa katika karatasi ya rangi ya njano.

(2) Kibali kilichotolewa chini ya kanuni ndogo ya (1) kitakuwa halali kwa muda wa miezi sita (6)

Vituo vya forodha

**19.-** (1) Mtu yeyote hataruhusiwa kuingiza dawa nchini isipokuwa kupitia vituo vya forodha vilivyoainishwa katika **Jedwali la Tisa** la Kanuni hizi.

(2) Mamlaka inaweza kubadili au kuongeza idadi ya vituo vya forodha vilivyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1), pale itakapobidi.

Masharti ya uingizaji na usafirishaji nje wa dawa za matumizi binafsi
Sura 311
Sura 319

**20.-** (1). Mamlaka inaweza kuidhinisha uingizaji au usafirishaji wa dawa nje ya nchi kwa matumizi binafsi baada ya kupokea maombi na kwa kiwango kinachokubalika.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), maombi ya uingizaji wa dawa kwa matumizi binafsi yatapaswa kuambatana na cheti cha dawa kutoka kwa daktari wa binadamu, daktari wa meno au daktari wa mifugo aliyesajiliwa.

(3) Isipokuwa kama masharti ya cheti cha dawa chini ya kanuni ndogo ya (2) yataainisha vinginevyo, mtalii au mgeni mwingine yeyote anayeingia nchini, au mkazi anayerudi nchini, anaweza kuingia na kiasi cha dawa kitakachotosha matibabu yake kwa muda wa siku ishirini na moja, ikiwa ni pamoja na mwenza au mtu mwingine anayesafiri naye.

Masharti ya dawa za msaada

**21.-** (1) Mtu yeyote hataruhusiwa kuingiza nchini dawa za msaada hadi atakapotimiza masharti ya Kanuni hizi.

(2) Mtu yeyote anayekusudia kuingiza dawa za msaada nchini, atapaswa kuwasilisha kwa Mamlaka maombi kwa njia ya kielektroniki kwa kujaza fomu iliyoainishwa kwenye **Jedwali la Tano** yakiambatana na cheti cha msaada na tozo kwa mujibu wa kanuni za ada na tozo zinazotumika.

(3) Maombi yaliyoainishwa chini ya kanuni ndogo ya (2), yatapaswa kuambatana na barua ya kuthibitisha msaada wa dawa husika kutoka idara, taasisi, wizara, au

mamlaka nyingine yoyote inayotambua msaada huo.

(4) Mamlaka inaweza baada ya kupokea maombi na kuridhika kuwa masharti ya Kanuni hizi yametimizwa, kuidhinisha uingizaji wa dawa za msaada na kutoa kibali kama ilivyoainishwa katika **Jedwali la Sita** la Kanuni hizi.

Uingizaji wa sampuli za dawa zisizouzwa

**22.-** (1) Mtu yeyote hataruhusiwa kuuza au kuhifadhi sampuli za dawa zisizouzwa.

(2) Kwa kuzingatia masharti mengine yaliyowekwa katika Kanuni hizi, uingizaji wa sampuli za dawa zisizouzwa utapaswa kufuata vigezo vifuatavyo:

(a) sampuli ziwekewe lebo yenye neno "HAIUZWI" kwa herufi kubwa na wino uliokolezwa);

(b) sampuli ziwe na ukubwa mdogo kulinganisha na sampuli zitakazouzwa kibiashara; na

(c) idadi ya sampuli isizidi 300 kwa kila shehena.

(3) Maombi yoyote ambayo hayatatimiza vigezo chini ya kanuni ndogo ya (2) yatatozwa tozo ya uingizaji dawa nchini.

Uingizaji wa dawa zisizotozwa

**23.-** (1) Kwa kuzingatia masharti mengine ya Kanuni hizi, maombi ya uingizaji wa dawa zisizotozwa yatapaswa kuaambatana na ankara kifani itakayoonesha bei ya kila dawa.

(2) Bila kuathiri masharti mengine ya Kanuni hizi, dawa zisizotozwa zitalipiwa tozo ya uingizaji dawa nchini kwa mujibu wa kanuni za ada na tozo zinazotumika.

Maombi ya kuingiza dawa za majaribio

**24.-** (1) Maombi ya uingizaji nchini wa dawa za majaribio ambayo yameidhinishwa na Mamlaka kufanyika Tanzania, yatawasilishwa na mfadhili au mtafiti mkuu wa majaribio.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), maombi yatapaswa kuwasilishwa pamoja na kibali cha kufanya majaribio ya dawa kilichotolewa na Mamlaka.

Muda wa matumizi wa dawa zinazoingizwa nchini

**25.** Mtu yeyote hataruhusiwa kuingiza dawa nchini ambayo muda wake wa matumizi uko chini ya asilimia 60 kwa dawa yenye muda wa matumizi unaozidi miezi ishirini na nne, na dawa ambayo muda wake wa matumizi uko chini ya asilimia 80 kwa dawa yenye muda wa matumizi ulio sawa au chini ya miezi ishirini na nne.

Uwekaji wa lebo kwenye dawa na mali ghafi zinazoingizwa nchini

**26.**- (1) Mtu yeyote atapaswa kuingiza nchini dawa yenye masharti ya lebo kama ilivyoainishwa kwenye kanuni za usajili wa dawa zinazotumika.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), malighafi za dawa zitapaswa kuwa na lebo yenye taarifa zifuatazo:

(a) jina halisi la kiambata hai;
(b) tarehe ya kutengenezwa na ya ukomo wa muda wa matumizi
(c) namba ya toleo au loti;
(d) masharti ya utunzaji;
(e) jina na anuani ya mtengenezaji; na
(f) uzito au ujazo.

(3) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya pili (2), lebo za malighafi ya dawa zitapaswa kuonekana, kutofutika, kuchapishwa moja kwa moja kwenye kifungashio, kusomeka na ziwe kwa lugha ya kiswahili au kiingereza.

(4) Bila kuathiri masharti ya Kanuni hizi, lebo za dawa za majaribio zitapaswa kuzingatia kanuni za majaribio ya dawa zinazotumika.

Kubatilisha, kufuta au kusimamisha kibali cha kuingiza au kusafirisha nje ya nchi

**27.** Mamlaka inaweza kubatilisha, kufuta au kusimamisha kibali cha kuingiza au kusafirisha dawa nje ya nchi kilichotolewa chini ya Kanuni hizi, endapo itajiridhisha kuwa mwingizaji, msafirishaji au shehena husika vimekiuka masharti ya Sheria au Kanuni hizi.

Ukaguzi wa shehena katika vituo vya forodha

**28.** (1) Dawa na malighafi hazitaruhusiwa kuondolewa katika kituo cha forodha hadi hapo zitakapokaguliwa na kuruhusiwa na mkaguzi.

(2) Shehena zote zitakazoruhusiwa na Idara ya Ushuru na Forodha kutolewa moja kwa moja kutoka kituo cha forodha kwenda kituo kingine chochote kwa ajili ya kuhifadhiwa, kituo hicho kitatambuliwa kama kituo cha forodha.

(3) Mwingizaji yeyote atapaswa kuonesha nyaraka zote muhimu wakati wowote zitakapohitajika na mkaguzi.

Uchukuaji wa sampuli

**29.** (1) Endapo italazimika au pale mkaguzi atashuku kuwa shehena ya dawa inakiuka masharti ya Sheria au Kanuni hizi, anaweza kuchukua sampuli kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), mkaguzi baada ya kukusanya sampuli atajaza fomu ya kuchukulia sampuli kama ilivyoainishwa katika **Jedwali la Kumi**.

Kukataa au kuzuia shehena

**30.-** (1) Endapo mkaguzi ataona ulazima wa kuharibu shehena, atawasilisha mapendekezo kwa Mamlaka.

(2) Amri yoyote ya kuteketeza dawa chini ya Kanuni hizi, itatekelezwa kwa mujibu wa kanuni za uondoaji kwenye soko na uteketezaji wa bidhaa zisizofaa

zinazotumika.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA JUMLA

Pingamizi

**31. -**(1) Mmiliki, mwingizaji au msafirishaji wa dawa au malighafi ambaye haridhiki na maamuzi yaliyotolewa na Mamlaka juu ya jengo au shehena yake anaweza kuwasilisha pingamizi lake akieleza sababu za kupinga maamuzi ya Mamlaka kwa maandishi kwa Mkurugenzi Mkuu au mtu yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi Mkuu kumwakilisha.

(2) Taarifa ya pingamizi kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) itatolewa ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe maamuzi yalipotolewa.

Mamlaka inaweza kuongeza muda wa kuwasilisha pingamizi usiozidi siku saba baada ya kuombwa na kupewa sababu za kutosha.

(3) Pale ambapo Mamlaka itapokea taarifa ya pingamizi kama ilivyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1), itateua mtu wa kushughulikia pingamizi hilo.

(4) Mtu aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (3) atapanga utaratibu utakaofuatwa kwa kuzingatia uzito wa pingamizi.

(5) Mtu aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (3) atapaswa kuzingatia maelezo ya pingamizi yaliyoandikwa au ya mdomo yaliyotolewa na mmiliki, mwingizaji au msafirishaji wa dawa au malighafi katika kushughulikia pingamizi lake, na atatoa mapendekezo kwa Mamlaka.

(6) Mapendekezo yatakayotolewa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (5) yatawasilishwa kwa maandishi kwa Mamlaka, na nakala kwa mtoa pingamizi au mwakilishi wake aliyemteua.

(7) Mamlaka itazingatia mapendekezo yaliyotolewa kwa kufuata kanuni ndogo ya (5).

(8) Mkurugenzi Mkuu atamjulisha ndani ya siku kumi na nne mmiliki, mwingizaji au msafirishaji wa dawa au malighafi endapo anakubali mapendekezo yaliyotolewa kwa kufuata kanuni ndogo ya (5), pale ambapo hakubaliani atatoa sababu za uamuzi huo.

(9) Maamuzi ya Mamlaka yataendelea kutekelezwa mpaka pale itakapoamuliwa vinginevyo wakati wa ushughulikiaji wa pingamizi hilo-

Rufaa

**32**.- (1) Bila kujali masharti ya kanuni ya 31, mtu yeyote ambaye

hajaridhika na uamuzi wa Mamlaka anaweza, ndani ya siku sitini tangu kupata nakala ya uamuzi, kukata rufaa kwa maandishi kwa Waziri.

(2) Mrufani atawasilisha nakala ya rufaa kwa Mamlaka, ambapo ndani ya siku kumi na nne Mamlaka itajibu kwa maandishi kwa Waziri na kumpa nakala ya majibu mrufani.

(3) Pale ambapo Waziri ana maoni kwamba kuna hoja ya kujibu, anaweza kuwaita wahusika kupata taarifa zaidi au kufanya uamuzi wa kuruhusu au kufuta rufaa.

Makosa na adhabu

**33**. Mtu yeyote anayekiuka au anayeshindwa kufuata Kanuni hizi moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja kumsaidia mtu mwingine kufanya kosa chini ya Kanuni hizi atakuwa na kosa na akitiwa hatiani, atapewa adhabu iliyowekwa kwa mujibu wa Sheria.

**34**.-(1) Mkurugenzi Mkuu, Mkaguzi au mtu mwingine yeyote aliyeidhinishwa anaweza, kwa kufuata na kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hizi, ikiwa ataridhika kwamba mtu ametenda kosa dhidi ya Kanuni hizi, atafifilisha kosa hilo kwa kupokea kutoka kwa mkosaji kiasi cha fedha ambacho kosa limetendwa.

(2) Kiasi cha fedha kitakacholipwa chini ya kanuni ndogo ya (1) kitakuwa ni theluthi mbili ya kiwango cha juu cha faini kwa kosa hilo kama ilivyoainishwa katika Sheria.

(3) Mamlaka ya kisheria yaliyotolewa na Kanuni hizi yatatumika pale ambapo mtuhumiwa atakiri kwamba ametenda kosa na anakubali kwa maandishi katika fomu ya kufifilisha makosa iliyoainishwa katika Kanuni za ada na tozo zinazotumika wakati huo.

(4) Mkurugenzi Mkuu au mkaguzi aliyepewa mamlaka ya kisheria chini ya kanuni hii atampa risiti baada ya kupokea malipo kutoka kwa mtu anayelipa kiasi cha fedha chini ya kanuni ndogo ya (2).

(5) Kiasi cha fedha chini ya kanuni hii kitalipwa kwa Mamlaka.

(6) Mtu yeyote akishtakiwa mahakamani kwa kosa lolote dhidi ya Kanuni hizi, itakuwa ni utetezi endapo mtu huyo atathibitisha kuwa kosa analoshitakiwa nalo lilifififilishwa chini ya kanuni hii.

MAJEDWALI

## JEDWALI LA KWANZA

| | | |
|---|---|---|
| | **MAOMBI YA USAJILI WA JENGO NA KIBALI CHA BIASHARA** | |

*(Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 5 (1))*

Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba,
P.O. Box 1253,
Dodoma, Tanzania.

**SEHEMU A: TAARIFA ZA MWOMBAJI**

Mimi / Sisi, naomba / tunaomba usajili wa jengo langu /letu jipya na kibali cha biashara kwa mujibu wa Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura 219

1. Jina la mwombaji ……………………………………………………………………………………
2. Anwani ya posta ………………………………………Namba ya simu……………………barua pepe ……………………………………………….

3. Kama ni
(a) * Kampuni; majina ya Wakurugenzi ..................................................................
(b) * Ushirika; majina ya Washirika ............................................. .........................................
(c) Ubia wa pamoja; jina la Chama na Wabia ..............................................
..................................

4. Mahali lililopo: ……………………………………………………………………
Namba ya kiwanja ……………………. Chombo au Nambari ya Lori ……………………Mtaa / Kijiji / Kata…………………… Wilaya / Manispaa/Jiji…………………………………………

5. Jengo litasajiliwa kwa biashara ya……………………………………………………
Biashara itakuwa chini ya Usimamizi wa Bw / Bi /Bibi/ Dkt / Prof (Jina Kamili) ……….ambaye ni Mfamasia/Daktari wa Mifugo mwenye namba ya usajili …………. ya mwaka…….na namba ya leseni ……………. (Tafadhali ambatisha nakala ya cheti cha usajili, namba ya leseni na makubaliano ya mkataba)

6. Jina la biashara ni …………………………………………

**SEHEMU B: TAMKO LA MWOMBAJI**

7. Mimi / sisi ................................................ hatujawahi kuhukumiwa kwa kosa lolote kwa mujibu wa Sheria inayozuia kufanya biashara yoyote chini ya Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura 219 au Sheria nyingine yoyote ile inayohusiana na biashara inayoombwa.

**ZINGATIA: Itakuwa ni kosa kutoa taarifa ya kupotosha au tamko la uwongo.**
Tarehe………………………………………..

Imesainiwa ……………………………………….

**Mwombaji**
* Ambatisha Cheti cha Usajili wa Kampuni/biashara

| | | |
|---|---|---|
| | **CHETI CHA USAJILI WA JENGO** | |

## JEDWALI LA PILI

**(Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 8 (1))**

Hii ni kuthibitisha kuwa jengo linalomilikiwa na M / S ………………………………………………. wa (Anwani ya Posta) ……………………ambalo liko kwenye kitalu namba .................. kiwanja namba....................... /Chombo / Lori namba………………………………….. lililopo kati ya ……… Mtaa...................................Kijiji / Kitongoji…………….. / Manispaa / Jiji……………, limesajiliwa kama……………………………na Nambari ya Usajili ……………………… .. ya 20 …

1. Kwa kuzingatia masharti yafuatayo: - Eneo au mahali ambapo biashara inafanyika lazima ifanane na mahitaji ya Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba Sura 219 au sheria nyingine yoyote inayohusiana na usajili wa majengo wakati wote vinginevyo cheti hiki kitasimamishwa au kufutwa
2. Mabadiliko yoyote katika umiliki, jina na eneo la jengo lililosajiliwa ni lazima yaidhinishwe na Mamlaka.
3. Cheti hiki hakiwezi kuhamishiwa kwa jengo jingine au kwa mtu mwingine yeyote
4. Cheti hiki kitawekwa wazi katika jengo lililosajiliwa.
5. Cheti kitatumika tu kuendesha biashara inayohusiana na bidhaa zilizoidhinishwa na TMDA.

……………………………………… ……………………………………………………

**Tarehe** **Sahihi ya Mkurugenzi Mkuu**

**Muhuri**

*: Futa yoyote ambayo haitumiki

| | | |
|---|---|---|
| | **KIBALI CHA BIASHARA** | |

## JEDWALI LA TATU

*(Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 8 (3))*

Nambari ya Kibali ………………………

Kibali anapewa M / S ......................................................................................................... wa S.L.P ……………………………………………………………… cha uingizaji na / usafirishaji ……………………………………………………………………………………………………….
katika jengo lililopo / kati ...................................................................Mtaa, kitalu/ kiwanja na…………../
Chombo / Lori namba……………………………………… Kijiji / Kitongoji …………………………Manispaa / Jiji …………………………………kwa namba ya usajili …………… ya 20 …………………….

Kibali hiki kitaanza kutumika kuanzia siku ambayo kitatolewa hadi kitakapomaliza muda wake tarehe 30 Juni ………………

Imetolewa tarehe ……………………………………… .. Ada iliyolipwa TZS …………………………………

Nambari ya Risiti ………………………………ya tarehe ………………………………………………………

……………………………………… ……………………………………………
**Tarehe** **Saini ya Mkurugenzi Mkuu**

muhuri

MASHARTI

1. Kibali hiki hakiidhinishi mmiliki kufanya biashara katika jengo ambalo halijasajiliwa au wakati wa kusimamishwa, kubatilishwa au kusitisha usajili wa eneo ambalo kibali kilitolewa.

| | | |
|---|---|---|
| | **MAOMBI YA KIBALI CHA KUINGIZA DAWA NCHINI** | TMDA Tanzania Medicines & Medical Devices Authority |

2. Kibali hiki hakiwezi kuhamishwa bila idhini ya maandishi ya Mamlaka.

NB: Futa yoyote ambayo haitumiki.

# JEDWALI LA NNE

*(Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 16 (1))*

Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba,
P.O. Box 1253,
Dodoma, Tanzania.

Mimi / Sisi ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... .. .. .. .. ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... …… ..

ya (anwani ya posta)................................... ninayefanya biashara ya uingizaji wa dawa /malighafi, ninaomba ombi kibali cha kuagiza dawa / malighafi nchini Tanzania kupitia kituo cha forodha cha……………………..

Namba ya Usajili wa Jengo ……………. ya mwaka………………………………………

Jina la Mfamasia Msimamizi ………………na namba ya usajili………………….na namba ya leseni ………………………….

Kusudi la idhini ya uingizaji: (weka alama pale inapofaa)

☐ Uingizaji wa malighafi / vifaa vya ufungaji kwa uzalishaji wa dawa za binadamu

☐ Uingizaji wa malighafi / vifaa vya ufungaji kwa uzalishaji wa dawa za mifugo;

☐ Uingizaji wa dawa binadamu;

☐ Uingizaji wa dawa mifugo;

☐ Uingizaji wa dawa za majaribio (ombi moja kwa kila dawa)

☐ Uingizaji wa Dawa kwa matumizi ya kibinafsi

☐ Nyingine.................................(taja)

Imeambatanishwa hapa na ankara ya kifani namba .. .. ... ... ... ... ... ya (tarehe) ... ... ...

**Tamko:**
Ninathibitisha kuwa maelezo niliyotoa katika fomu ya maombi na ankara kifani ni ya kweli na sahihi.

Tarehe ya maombi ... ... ... .............................

Saini ya Mfamasia / Daktari wa Mifugo Msimamizi............................

Muhuri …………………....

**Kwa matumizi Ofisi tu:**

Imepokelewa na: ..................................... Sahihi................................

Muhuri....................................

| | | |
|---|---|---|
| | **MAOMBI YA KIBALI CHA USAFIRISHAJI WA DAWA NJE YA NCHI** | TMDA Tanzania Medicines & Medical Devices Authority |

## JEDWALI LA TANO

*(Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 16 (2))*

Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba,
P.O. Box 1253,
Dodoma, Tanzania.

Mimi/sisi … … … … … … … … … … … … … … .. .. .. .. … … … … … … … … … … … … …… ..

ya (anwani ya posta)................................... ninayefanya biashara ya kusafirisha dawa / malighafi nje ya nchi, ninaomba kibali cha kusafirisha nje ya nchi dawa / malighafi kupitia kituo cha forodha cha……………………..

Namba ya Usajili wa Jengo ……………. ya mwaka………………………………………
Jina la Mfamasia Msimamizi ………………na namba ya usajili………………….na namba ya leseni …………

Jina la Mpokeaji ........................................................................................................anuani / Mahali shehena inapokwenda ......…………… .. Jina la nchi ………………………………………………

Kusudi la ruhusa ya kusafirisha nje: (weka alama pale inapofaa);
☐ Usafirishaji wa dawa kwa matumizi ya binadamu;
☐ Usafirishaji wa dawa kwa matumizi ya mifugo;
☐ Usafirishaji wa dawa za majaribio
☐ Usafirishaji wa malighafi na / au vifungashio vya dawa za binadamu;
☐ Usafirishaji wa malighafi na / au vifungashi vya dawa za mifugo;
☐ Nyingine yoyote (Taja) ………………… .. ……………………………………………
Imeambatishwa na ankara kifani …………………………… ya tarehe ... ... ... ...

**Tamko:**
Ninathibitisha kuwa maelezo niliyotoa katika fomu ya maombi na ankara kifani ni ya kweli na sahihi.

Tarehe ya maombi ... ... ... ... ... ............................
Saini ya Mfamasia / Daktari wa Mifugo Msimamizi .........................................
Muhuri ………………… ....

**JEDWALI LA SITA**

| | **KIBALI CHA KUINGIZA DAWA NCHINI** | |
|---|---|---|

*(Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 17 (2))*

**Nambari ya Kibali: TMDA........................**

**<u>SEHEMU A:</u>**

Jina la mwingizaji aliyesajiliwa .................... Anuani ya posta .................. Namba ya simu.........

Nchi dawa au malighafi zinapotoka ......................Namba ya ankara ...................... Tarehe

Jina la Msafirishaji / Mtumaji ..................................  Anuani ya posta .......................................

Kuwasili kunatarajiwa kwa meli / anga / nchi kavu, kupitia kituo cha forodha cha ……………

| **S / N.** | | | | **Dawa / Malighafi** | **Kiasi kilichope wa kibali** | **Thamani ya dawa** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Jina Halisi la Dawa** | **Jina la kibiash ara la dawa** | **Toleo Na.** | **Nambari ya usajili** | | |
| | | | | | | |

**JUMLA:**

<u>Ada</u> <u>Stakabadhi Na.</u> <u>Tarehe</u>

............................................... ............................................... ...................................

**SEHEMU B:**

Idhini imetolewa kuingiza nchini dawa / malighafi zilizotajwa. Mwingizaji atalazimika kuhakikisha kuwa dawa au malighafi zinakaguliwa na mkaguzi wa TMDA katika kituo cha forodha kabla ya kuruhusiwa kutolewa katika kituo hicho.

Tarehe **Kny: Mkurugenzi Mkuu na Muhuri**

.............................................. .............................................. .........................................

**SEHEMU C:**

Mimi____________________nikiwa mkaguzi wa TMDA katika kituo cha forodha cha ………nimekagua dawa / malighafi zilizoorodheshwa hapo juu na kuona zinafaa / hazifai kwa matumizi yaliyokusudiwa hivyo ninaruhusu/siruhusu kuingizwa nchini.

____________________________ ______________________________

**Tarehe** **Saini ya TMDA**

**Muhuri**

Zingatia:

1. Kibali hiki ni cha shehena moja tu na kitadumu kwa miezi sita kuanzia tarehe ya idhini.
2. Mkaguzi lazima aingize taarifa za shehena katika mfumo wa kielektroniki mara moja na kurudisha nakala ya kibali TMDA.

**JEDWALI LA SABA**

| | | |
|---|---|---|
| | **KIBALI CHA KUSAFIRISHA DAWA NJE YA NCHI** | TMDA Tanzania Medicines & Medical Devices Authority |

*(Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 17 (3))*

Kibali Na........................... Tarehe………………..

Jina la Msafirishaji......................
Sanduku la posta................................
Mkoa ………………….............

**YAH: KIBALI CHA KUSAFIRISHA DAWA KUTOKA TANZANIA KWENDA ……… KAMPUNI, JINA LA NCHI …………………….**

Rejea inafanywa kwa barua yako ya maombi iliyopokelewa mnamo ................ iliyoambatishwa na nambari ya ankara kifani …… .. ya tarehe.............. ..............

Kwa kuzingatia sheria zingine zinazosimamia biashara ya kuuza nje, kibali kimetolewa kwa ..............................., chini ya kifungu 73 (1) cha Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura ya 219 kusafirisha dawa/malighafi zifuatazo kwa............... ………………… .. JINA LA NCHI

| **Na.** | **Dawa** | **Bei kwa kiasi cha kipimo** | **Kiasi** | **Thamani ya dawa** |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

**JUMLA:**

Ruhusa inapewa kusafirisha dawa/malighafi zilizotajwa. Kibali hiki kitatumika kutoka tarehe …. ......... ............... mpaka ……….. …................

__________________ ________________________

Tarehe **KNY: MKURUGENZI MKUU**

**UJUMLA**

Zingatia
: 1. Kibali hiki ni cha shehena moja tu na kitatumika kwa miezi mitatu kuanzia tarehe ya ruhusa.
2. Mkaguzi lazima arudishe mara moja nakala iliyokamilishwa ya kibali hiki pamoja nanakalaya cheti cha kutolewa kwa TMDA.

**JEDWALI LA NANE**

| | | |
|---|---|---|
| | **KIBALI CHA KUINGIZA/KUSAFIRISHA DAWA ZA TIBA ZENYE ASILI YA KULEVYA** | TMDA<br>Tanzania Medicines & Medical Devices Authority |

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 18 (1))*

*Namba ya mfuatano* ______________________________
*Namba ya faili*___________________________________

Mimi mwenye dhamana niliyopewa kwa mujibu wa Sheria kutoa kibali cha dawa za tiba zenye asili ya kulevya za nakotiki/ saikotropiki au kemikali bashirifu na kwa mujibu wa Makubaliano ya Kimataifa ya Dawa za Tiba zenye Asili ya kulevya, nathibitisha kuwa nimetoa idhini ya uingizaji wa
________________________________________________________________________ ya

________________________________________________________________________

Kutoka _________________________________________________________________

Kwa masharti yafuatayo:

i. Shehena itaingizwa kabla ya ____________________________________________ na
ii. Shehena itaingizwa na _________________________________________________
iii. Kupitia ______________________________________________________________

Na kwamba nimeridhika kuwa shehena inayoombewa kibali cha kuingizwa nchini inahitajika kwa matumizi ya tiba na kisayansi tu.

____________________________ ____________________________________
Saini na muhuri wa Mkurugenzi Mkuu

**Angalizo**: Nyaraka hii ni kwa ajili ya matumizi pekee ya Serikali ya nchi ambapo dawa zinatolewa.

**JEDWALI LA TISA**

| | | |
|---|---|---|
| | **VITUO VYA FORODHA VILIVYOIDHINISHWA** | |

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 19 (1))*

Dawa zitakazoingizwa au kusafirishwa nje ya nchi ya Tanzania zitaruhusiwa kupitia vituo vya forodha vifuatavyo

1. Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere
2. Bandari ya Dar es Salaam
3. Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro
4. Horohoro
5. Holili
6. Namanga
7. Sirari
8. Bandari ya Ziwa Viktoria Mwanza
9. Uwanja wa Ndege wa Mwanza
10. Bandari ya Tanga
11. Tunduma
12. Mtukula
13. Rusumo
14. Kabanga
15. Kasumulo

Mamlaka ina haki ya kuamua uingizaji au usafirishaji nje ya nchi wa dawa kupitia kituo cha forodha zaidi ya vilivyotajwa.

**JEDWALI LA KUMI**

| | | |
|---|---|---|
| | **FOMU YA KUCHUKUA SAMPULI** | TMDA Tanzania Medicines & Medical Devices Authority |

*(Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 29 (2))*

1. Nambari ya sampuli: .............................................. ...............
   (Mkoa / dawa / nambari ya mfuatano / tarehe ya sampuli: siku/mwezi/mwaka)
2. Jina la jengo ambapo sampuli ilichukuliwa: .......................................................
3. Anuani ya jengo .................................... ...... Anuani ya posta ............................
   Namba ya simu ..................................... Namba Nukushi ................................ .................
   Barua pepe...........................................(kama ipo)
4. Jina la sampuli ya dawa: ........................................
5. Jina la viambata hai vya dawa na nguvu: ................................................
   .............................................. ........
6. Muundo wa dozi (kidonge, poda ya kinywa nk): ............................
7. Ukubwa wa kifungashio na aina: ........................................... .....................
8. Namba ya toleo / loti: .............. Tarehe ya kutengenezwa: ............. Tarehe ya kumaliza muda wa matumizi:.........
9. Jina na anuani ya mtengenezaji:
   ............................................... ................................................ .....................
10. Idadi ya sampuli zilizochukuliwa .........................
11. Je! dawa hiyo imesajiliwa Tanzania? Ndiyo / Hapana. Kama Ndiyo, Jaza namba ya usajili: .........................................
12. Toa maoni kuhusu hali ya uhifadhi wa dawa katika jengo hilo: ...............................
    ............................................... ................................................ .....................
    ............................................... ................................................ .....................
13. Jina na saini ya mwakilishi wa jengo ambapo sampuli ilichukuliwa:
    Jina .................................. .................Saini................................ ......Tarehe…………
14. Jina la mkaguzi wa Dawa / Mchukuaji wa Sampuli

| Na. | Jina | Taasisi | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |

**Kumbuka:** **Sampuli zilizochukuliwa ni sharti ziwe katika kifungashio halisi**

Dodoma,
……. …………….., 2025

**MOHAMED OMARY MCHENGERWA**
*Waziri wa Afya*